**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA SITA

**09 FEBRUARI, 2021**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA SITA – TAREHE 09 FEBRUARI, 2021

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI MKUU:**

(Magazeti ya Serikali na Nyongeza zake)

1. Toleo Na. 14 la tarehe 03 Aprili, 2020;
2. Toleo Na. 15 la tarehe 10 Aprili, 2020;
3. Toleo Na. 16 la tarehe 17 Aprili, 2020;
4. Toleo Na. 17 la tarehe 24 Aprili, 2020;
5. Toleo Na. 18 la tarehe 01 Mei, 2020;
6. Toleo Na. 19 la tarehe 08 Mei, 2020;
7. Toleo Na. 20 la tarehe 15 Mei, 2020;
8. Toleo Na. 21 la tarehe 22 Mei, 2020;
9. Toleo Na. 22 la tarehe 27 Mei, 2020;
10. Toleo Na. 23 la tarehe 05 Juni, 2020;
11. Toleo Na. 24 la tarehe 12 Juni, 2020;
12. Toleo Na. 25 la tarehe 19 Juni, 2020;
13. Toleo Na. 26 la tarehe 26 Juni, 2020;
14. Toleo Na. 27 la tarehe 03 Julai, 2020;
15. Toleo Na. 28 la tarehe 10 Julai, 2020;
16. Toleo Na. 29 la tarehe 17 Julai, 2020;

17. Toleo Na. 30 la tarehe 24 Julai, 2020;
18. Toleo Na. 31 la tarehe 31 Julai, 2020;
19. Toleo Na. 32 la tarehe 07 Agosti, 2020;
20. Toleo Na. 33 la tarehe 14 Agosti, 2020;
21. Toleo Na. 34 la tarehe 21 Agosti, 2020;
22. Toleo Na. 35 la tarehe 28 Agosti, 2020;
23. Toleo Na. 36 la tarehe 04 Septemba, 2020;
24. Toleo Na. 37 la tarehe 11 Septemba, 2020;
25. Toleo Na. 38 la tarehe 18 Septemba, 2020;
26. Toleo Na. 39 la tarehe 25 Septemba, 2020;
27. Toleo Na. 40 la tarehe 02 Oktoba, 2020;
28. Toleo Na. 41 la tarehe 09 Oktoba, 2020;
29. Toleo Na. 42 la tarehe 16 Oktoba, 2020;
30. Toleo Na. 43 la tarehe 23 Oktoba, 2020;
31. Toleo Na. 44 la tarehe 30 Oktoba, 2020;
32. Toleo Na. 45 la tarehe 06 Novemba, 2020;
33. Toleo Na. 46 la tarehe 13 Novemba, 2020;
34. Toleo Na. 47 la tarehe 20 Novemba, 2020;
35. Toleo Na. 48 la tarehe 27 Novemba, 2020;
36. Toleo Na. 49 la tarehe 04 Disemba, 2020;
37. Toleo Na. 50 la tarehe 11 Disemba, 2020;
38. Toleo Na. 51 la tarehe 18 Disemba, 2020;
39. Toleo Na. 52 la tarehe 25 Disemba, 2020;
40. Toleo Na. 01 la tarehe 01 Januari, 2021;
41. Toleo Na. 02 la tarehe 08 Januari, 2021;
42. Toleo Na. 03 la tarehe 15 Januari, 2021;
43. Toleo Na. 04 la tarehe 22 Januari, 2021; na
44. Toleo Na. 05 la tarehe 29 Januari, 2021.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

## III. MASWALI:

### WAZIRI MKUU:

**73. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kituo cha Uwekezaji (TIC) kinampa haki Mwekezaji kuajiri Watalaam lakini upande wa pili Sheria inampa mamlaka Kamishna wa Kazi kufanya maamuzi kuhusu maombi ya vibali vya kazi:-

Je, ni lini Serikali italeta marekebisho ya Sheria ili kuondoa mgongano huo.

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**74. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa Kujenga Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

**75. MHESHIMIWA NICODEMUS HENRY MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga chumba cha kuhifadhia maiti kwenye Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**76. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa Wananchi wa Manispaa ya Bukoba kuwa wanufaika wa TASAF ni Wananchi wenye uwezo badala ya kaya maskini:-

Je, hayo ndiyo malengo ya kuanzishwa kwa TASAF.

**77. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi aliyoitoa Mhe. Rais wakati wa kampeni ya kuongeza Watumishi 403 wa Afya.

**WIZARA YA MAJI:**

**78. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Tarime utakamilika.

**79. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini utekelezaji wa mradi wa maji kwa Vijiji 57 vya Wilaya ya Kyerwa utaanza kwa kuwa usanifu wa kina wa mradi huo umeshakamilika.

**80. MHESHIMIWA YAHYA ALLY MHATA (NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kwenda Mji wa Mangaka utaanza.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**81. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Likuyufusi Mkenda yenye urefu wa Km 124 kwa kiwango cha lami ili kufungua zaidi fursa za kiuchumi kati ya nchi yetu na Msumbiji.

**82. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Lupiro – Malinyi – Londo – Namtumbo yenye urefu wa Kilometa 296 ambayo ipo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020.

**83. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa kipande cha barabara kutoka Mbagala Zakhiem hadi Mbagala Kuu na kipande cha barabara toka Mbande Kisewe hadi Msongola.

**WIZARA YA KILIMO:**

**84. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Mfumo wa ununuzi wa kahawa kupitia Vyama vya Ushirika umekuwa mwiba kwa Wananchi wa Kyerwa na Karagwe kupitia KDCU; kiasi cha kufikia hadi miezi 6 bila Wananchi kulipwa fedha zao:-

(a) Je, kwanini Serikali isiruhusu watu binafsi kununua Kahawa moja kwa moja kutoka kwa Mkulima;

(b) Je, ni lini Wakulima wanaodai fedha zao watalipwa.

**85. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza mazingira wezeshi ya

kuongeza bei ya zao la Kahawa ili Wakulima wa zao hilo waweze kunufaika;

(b) Utaratibu wa ununuzi wa zao la Kahawa unapitia Vyama vya Ushirika hali inayoonekana kutovutia ushindani. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi ili kuvutia ushindani.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**86. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Jimbo la Tunduru Kusini limepakana na Nchi ya Msumbiji kwa upande wa Kusini:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Uhamiaji na cha Polisi ili kuhudumia maeneo hayo ya Mpakani.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**87. MHESHIMIWA FELISTER DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itatoa hati kwa Wananchi wa Meko na Basihaya baada ya maeneo hayo kupimwa.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/22 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **S. KAGAIGAI**
**09 FEBRUARI, 2021** **KATIBU WA BUNGE**